

Na: 19. Msimu wa Kilimo 2018/19 Tathmini ya Kipindi cha Aprili 01-10, 2019 na Matazamio kwa Kipindi cha Aprili 11-20, 2019

Muhtasari


- Mvua za msimu zinazoendelea zitasaidia kuongeza unyenyevu kwenye udongo ambao utasaidia ukuaji wa mazao.
- Wakulima, wafugaji na wavuvi wanashauriwa kufuata ushauri unaotolewa na maafisa ugani ili kuongeza uzalishaji wenye tija kutokana na mvua zinazotarajiwa.

**MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA
KIPINDI CHA APRILI 01-10, 2019**

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia na ile iliyopo kusini, (Azore na Siberia na St. Helena na Mascarene) ilidhoofika. Hali hii ilisababisha msukumo wa ukanda wa mvua Inter-Tropical Convergence Zone (ITCZ) kuwepo katika maeneo mengi ya Tanzania. Joto la bahari la juu ya wastani liliendelea katika eneo la magharibi mwa bahari ya Hindi pia joto la chini ya wastani katika eneo la Rasi ya Msumbiji hali iliyosababisha, kufanyika kwa mgandamizo mdogo wa hali ya hewa na makutano ya upepo nje kidogo ya ukanda wa bahari ya Tanzania. Katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi joto la bahari lilikua juu ya wastani hivyo kuchangia katika kufanyika kwa vimbunga baharini. Joto la bahari la juu kidogo ya wastani lilikuwa katika eneo la kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola). Hali hii ilisababisha mabadiliko makubwa ya mifumo ya hali ya hewa katika maeneo ya magharibi mwa nchi.

**MWENENDO WA MVUA KATIKA KIPINDI CHA
APRILI 01-10, 2019**

Kutokana na mifumo ya hali ya hewa katika kipindi cha tarehe 1 hadi 10 Aprili 2019, mvua ziliongezeka katika baadhi ya maeneo ya nyanda za juu kusini magharibi, kusini, ukanda wa Pwani, kanda ya ziwa Victoria na magharibi. Maeneo haya yalipata mvua kati ya mm 26 na 100. Hata hivyo maeneo ya mkoa wa Ruvuma, Mara, Simiyu na Morogoro yalipata mvua za zaidi ya mm 150. Maeneo mengine hususan kanda ya kati na nyanda za juu kaskazini mashariki yalipata mvua chini ya mm 10 kama Kielelezo kinavyoonyesha.



Kielelezo:1: Kiasi cha mvua katika kipindi cha April 01- 11, 2019.

**TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA
KIPINDI CHA APRILI 01-10, 2019**

Katika kipindi cha siku kumi maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua hususan mkoa wa Mbeya, Iringa, Rukwa, Ruvuma zao la mahindi lilikuwa katika hali nzuri na hatua ya kukomaa. Hata hivyo zao la mahindi limeathiriwa katika maeneo ya kanda ya kati kutokana na upungufu wa mvua. Maeneo yanayopata mvua mara mbili kwa mwaka kama vile Simiyu, Mwanza na Shinyanga wakulima wanaendelea na shughuli za uvunaji. Kutokana na upungufu wa mvua za Vuli na kuchelelewa na mvua za Masika, mazao ya msimu hayakuwa katika hali nzuri isipokuwa mkoa wa kagera hususan Bukoba ambapo wameendelea kupata mvua ambazo zimesaidia ukuaji wa mazao.

HALI YA MAJI ILIVYOKUWA KATIKA KIPINDI CHA APRILI 01-10, 2019

Kina cha maji katika mabwawa na mitiririko ya maji kwenye mito kwa maeneo yaliyoendelea kupata mvua kiliendelea kuongezeka kutokana na mvua zilizoendelea kunyesha.

MIFUMO YA HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA APRILI 11-20, 2019

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia na ile iliyopo kusini, (Azore na Siberia na St. Helena na Mascarene) iliidhofika. Hali hii ilisababisha msukumo wa ukanda wa mvua Inter-Tropical Convergence Zone (ITCZ) kuwepo katika maeneo mengi ya Tanzania. Joto la bahari la juu ya wastani liliendelea katika eneo la magharibi mwa bahari ya Hindi pia joto la chini ya wastani katika eneo la Rasi ya Msumbiji hali iliyosababisha, kufanyika kwa mgandamizo mdogo wa hali ya hewa na makutano ya upepo nje kidogo ya ukanda wa bahari ya Tanzania. Katika eneo la kusini- magharibi mwa bahari ya Hindi joto la bahari lilikua juu ya wastani hivyo kuchangia katika kufanyika kwa vimbunga baharini. Joto la bahari la juu kidogo ya wastani lilikuwa katika eneo la Kusini-mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola). Hali hii ilisababisha mabadiliko makubwa ya mifumo ya hali ya hewa katika maeneo ya magharibi mwa nchi.

HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA APRILI 11-20, 2019

Katika kipindi hiki maeneo ya kanda ya ziwa Victoria (mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara) yanatarajiwa kupata mvua zinazoambatana na ngurumo. Nyanda za juu kaskazini mashariki (mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro) yanatarajiwa kupata mvua zinazoambatana na ngurumo, hususani nusu ya pili ya dekad. Pwani ya kaskazini (mikoa ya Tanga, Maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba) yanatarajiwa kupata mvua zinazoambatana na ngurumo katika

maeneo machache. Magharibi mwa nchi (mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora) kunatarajiwa kupata mvua zinazoambatana na ngurumo katika maeneo machache, hususani nusu ya kwanza ya dekad. Kanda ya kati (mikoa ya Dodoma na Singida) yanatarajiwa kupata hali ya ukavu. Nyanda za juu kusini magharibi (mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa), kanda ya kusini (mkoa wa Ruvuma na Maeneo ya kusini mwa Morogoro) na Pwani ya kusini (mikoa ya Mtwara na Lindi) yanatarajiwa kupata mvua zinazoambatana na ngurumo katika baadhi ya maeneo.

MATARAJIO NA USHAURI KWA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA APRILI 11-20, 2019

Unyevunyevu kwenye udongo unatarajiwa kuongezeka hususan maeneo ya nyanda za juu kusini magharibi, pwani ya kusini, kanda wa ziwa Viktoria, nyanda za juu kaskazini mashariki, pwani ya kaskazini, maeneo ya kusini na magharibi mwa nchi kutokana namvua zinazotarajiwa. Hali hii itasaidia ukuaji wa mazao. Hali ya ukavu inavyotarajiwa katika maeneo ya kanda ya kati itaendelea kuathiri ukuaji wa mazao ya msimu. Wakulima, wafugaji na wavuvi wanashauriwa kuendelea kufuata ushauri unaotolewa na maafisa ugani ili kuongeza tija kutokana na mvua zinazotarajiwa

HALI YA MAJI INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA APRILI 11-20, 2019.

Kina cha maji kwenye mabwawa na mitiririko wa maji kwenye mito vinatarajiwa kuendelea kuongezeka katika sehemu nyingi nchini. Hata hivyo, wananchi wanashauriwa kutumia maji hayo kwa uangalifu hususan maeneo ambayo yametabiliwa kuwa na upungufu wa mvua kama maeneo ya kati (Dodoma & Singida).

Jarida limetayarishwa na:

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania
Ghorofa ya 3-Ubungo Plaza – Barabara ya Morogoro, Dar es Salaam-Jamhuri ya Muungano wa Tanzania